

Wapendwa Wazazi,

Mojawapo ya ujumbe muhimu wa Agano Jipya ni kwamba tunaweza kupata amani na furaha katika Kristo, licha ya hali ya maisha yetu. Jarida la mwezi huu linashiriki ushuhuda sawa na huu.

- Kwenye ukurasa wa R4, mvulana anapata faraja baada ya kuota ndoto mbaya.
- Kwenye ukurasa wa R8, msichana mwenye Down syndrome anakumbushwa kwamba Baba wa Mbinguni anampenda.
- Kwenye ukurasa wa R15, bango linafundisha kwamba mambo yote yanawezekana kwa msaada wa Yesu Kristo.
- Kwenye ukurasa wa R20–23, Paulo anaweka mfano wa imani.


Mnaposoma jarida hili pamoja, tafuteni jinsi Yesu na Baba wa Mbinguni walivyowasaidia watu katika kila hadithi. Ungeweza kupigia mstari maneno ambayo yanaelezea changamoto walizopata. Kisha zungushia duara maneno ambayo yanaelezea usaidizi upi walipokea. Kama familia, zungumzeni kuhusu jinsi wakati mwingine majaribu yanavyoondolewa, na wakati mwingine tunavyofanywa imara kuvumilia majaribu yetu. Vyovyote vile, Yesu na Baba wa Mbinguni wanatupenda na wapo kwa ajili yetu!

Tunatumaini mmekuwa na mwezi wenye furaha,

Rafiki

Jinsi ya Kutuma Kazi ya Sanaa ya Mtoto Wako kwenye Liahona

Nenda kwenye liahona.ChurchofJesus Christ.org na ubofye “Wasilisha Makala au Jibu.” Au itume kwa barua pepe kwa liahona@ChurchofJesusChrist.org likiwemo jina la mtoto wako, umri, jiji la makazi, na maelezo haya ya ruhusa: “Mimi, [ingiza jina lako], natoa ruhusa kwa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho kutumia wasilisho la mtoto wangu kwenye majarida ya Kanisa, kwenye mitandao ya Kanisa, na kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii.” Tuna hamu ya kusikia kutoka kwako!



Tafuta Liahona iliyofichwa ndani!

YALIYOMO

- R2** Kuwapenda Wengine kama Yesu Anavyotupenda
- R4** Umbali wa Sala Tu
- R6** Halo kutoka Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo!
- R8** Sitaki Kuwa Tofauti.
- R10** Mitume kote Ulimwenguni: Mzee Stevenson Anazuru Chile
- R11** Mitume kote Ulimwenguni: Mzee Renlund Anawatembelea Watoto
- R12** Kofia Nyeupe kwa ajili ya Florence
- R14** Je, Ninapaswa Kuendelea Kusoma?
- R15** Wazo Zuri: Nayaweza mambo yote katika Kristo
- R16** Changamoto ya Hekalu
- R17** Onyesha na Sema
- R18** Mifano ya Ujasiri: Kumtumikia Bwana kwa Kihispania
- R20** Hadithi za Maandiko: Safari za Umisionari za Paulo
- R23** Ukurasa wa Kupaka Rangi: Yesu Anaweza Kunisaidia Kufanya Mambo Magumu

JUU YA JALADA LA RAFIKI
Kielelezo na Macky Pamintuan